



1 Novemba 2016

## SERIKALI, BUNGE NA WADAU WA HABARI WASIKILIZANE

Kwa takribani wiki mbili sasa kumekuwepo na majibizano kupitia vyombo vya habari baina ya Msemaji wa Serikali na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za jamii kwa upande mmoja; na wadau wa habari na vyombo vya habari kwa upande wa pili.

Majibizano haya yamehusu **Mswada wa Sheria ya Huduma za Habari wa 2016**. Upande wa Serikali na Bunge kwa pamoja wamesimamia hoja kwamba mswada huo umejadiliwa na wadau tangu 1993. Kwamba ulipelekwa bungeni mwaka jana kwa hati ya dharura wadau wakaomba muda zaidi hivyo ukaondolewa. Madai mengine ni kwamba sasa hauwezi kusubiri tena, lazima upitishwe.

Wadau wa habari nao wamekiri kushiriki katika mchakato huo tangu 1993 na kwamba wanahitaji sheria hiyo ipitishwe lakini wanaomba muda zaidi ili waweze kushirikisha wadau wengine katika mikoa mbalimbali nchini, kujadili na kutoa mapendekezo. Wanadai kuna maudhui mapya ambayo wadau wanahitaji muda kujadiliana na kukubaliana. Kwamba, wamesubiri miaka yote hiyo, hivyo haitokuwa na maana kuharakisha bila ridhaa na maelewano ya wadau wote wa habari.

Sikika inaamini pande zote mbili zina nia moja; kutengeneza sheria itakayosimamia huduma za habari kwa weledi, haki, na ufanisi. Serikali inataka kuupitisha sasa wakati wadau wanaomba upitishwe kwenye Bunge la Februari 2017 ili kupata muda wa kutosha kuridhia maudhui mapya ya mswada huo.

Kwa kuwa hadi sasa pande zote mbili hazijapishana sana kwenye maudhui, muda wa miezi mitatu usisababishe dosari kwenye maelewano na mahusiano ya muda mrefu, tangu kuanza kwa mchakato huo. Serikali, Bunge, vyombo vya habari na wanahabari wanategemeana sana katika kutimiza majukumu yao kwa umma.

Kwa maoni yetu, wananchi na asasi za kiraia ni wanufaika wa maelewano na ushirikiano baina ya pande hizo husika. Tunapenda kuona kasi na tija kuelekea kwenye maendeleo ya pamoja badala ya kusigana na kutunishiana misuli. Hivyo, tunashauri mswada huu usogezwe mbele hadi Februari 2017 ili unufaikie na ushiriki mpana wa wadau wa habari, na hivyo kuendeleza na kuboresha maelewano ya pande zote husika, kwa manufaa ya watanzania.

Bw. Irenei Kiria  
Mkurugenzi wa Sikika,  
S.L.P 12183 Dar es Salaam,

Simu: +255 222 666355/57, Fax: 2668015, Email: info@sikika.or.tz, Website: www.sikika.or.tz